

“Everyone’s Different – Respect for Minorities”

Episode 08:

The San in Botswana and Their Fight for Land and Water

Autor: Adrian Kriesch (HA Afrika) – 4945

Editor: Katrin Ogunsade

Translator: Charlotte Collins

O-Töne. Botswana Clips Minorities (LbE Prod.)

Characters

<i>Narrator</i>	m`mume/m`mke	miaka 30	english
<i>Roy Sesana</i>	m`mume	zaidi ya miaka 60	san
<i>Jumanda Gakelebone</i>	m`mume	kiasi miaka 35	english
<i>Sithilo Thekiso</i>	m`mume	kiasi miaka 45	san
<i>Mosalagadi Mowawaphuti</i>	m`mke	kiasi miaka 45	english
<i>Mabele Owa</i>	m`mume	kiasi miaka 60	san

Intro

Hujambo na karibu kwenye sehemu ya nane ya kipindi chetu cha **Noa Bongo Jenga Maisha Yako**, “**Kila mtu ni tofauti-Kuzingatia maslahi ya jamii za walio wachache**”. Katika kipindi chote hiki tutakutana na watu kadha wa kadha, walio tofauti na watu wengine katika jamii wanamoishi, wanavyoonekana na wanavyoelewa mambo. Huwa ni kawaida kwao kubaguliwa, lakini wanajitahidi kutetea haki zao. Leo tunakwenda Botswana kukutana na kundi la wakazi wa asili. Wasanambao ni jamii ya wawindaji-wahamaji– wameishi katika sehemu ya kati ya jangwa la Kalahari kwa maelfu ya miaka. Wanasemekana kuwa ndio watu wa kwanza kuwepo barani Afrika. Miaka kadhaa iliyopita, serikali ilitaka kuwalazimisha wahame kwenye ardhi yao. Hawakuungama hivi hivi; badala yake walijitetea kwa njia ya amani wakafaulu kupata haki ya kumiliki ardhi na maji.

Text

1. Clip Roy Sesana (San)

“Jina langu ni Roy Sesana na nina umri wa miaka zaidi ya 60. Nilizaliwa katika eneo hili la Kalahari, sawa na babu yangu, baba yangu na ndugu zangu. Tunaishi kwenye ardhi nzuri tambarare, na iliyo wazi. Mandhari hupendeza zaidi katika majira ya mvua; wakati huo kuna maua mengi. Nyinyi watu wa mijini mna maduka ambapo mnaweza kununua kila kitu. Hapa mwituni ninaweza kupata kila kitu pia. Ninaweza kupata mizizi ninapokuwa na njaa, au matikiti. Ninaweza pia kuwinda. Ningependa vitukuu vyangu viishi katika eneo hili.”

2. SFX: Roy shows us his hut

3. Narration

Roy ana furaha si haba anaponionyesha mahali anapoishi. Eneo hili la makazi ya nyumba ndogo za msonge linaitwa Molapo na limo katika Mbuga ya Kitaifa ya Wanyama katikati ya Jangwa la Kalahari. Hali ya hewa ni yabisi na kuna upepo mkali. Roy anaturalika kwenye nyumba yake, ilizojengwa kwa miti na matawi na imezekwa kwa minyaa. Ana furaha si haba kwamba anaishi tena katika eneo hili. Ni jambo ambalo alilipigania sana na kwa muda mrefu. Mwaka 1997, wakazi wa mbuga hiyo ya kitaifa walihamishwa kwa nguvu. Serikali ya Botswana ilidai kwamba wanyamapori wasingekuwa salama katika mbuga iwapo watu wangeendelea kuishi humo. Roy pamoja na wanaharakati wengine wa kisiasa walikata rufaa mara kadhaa dhidi ya uamuzi huo – mwaka 2006 wakashinda kesi. Wakazi wa asili wakaruhusiwa kurudi kwenye makazi yao. Kesi hiyo ilifuatiliwa kwa kina kote duniani. Uamuzi huo ukawa na manufaa si kidogo kwa jamii ya Wasan. Lakini kama asemavyo Roy, masahibu yao hayakuishia hapo.

4. Clip Roy Sesana (San)

“Ingawa mahakama iliamua kwamba turuhusiwe kisheria kuishi katika ardhi yetu, serikali bado inatusumbua. Sisi ni wawindaji lakini hatuna wanyama wengi wa kuwinda. Walituhidi kwamba wangetupa vibali maalumu vya kuwinda, lakini hatukuvipata. Hawatupatii huduma za

msingi kama vile maji safi na salama. Tulipata maji baada ya kuishtaki serikali mahakamani.”

5. Narration

Kipande cha ardhi ambacho Roy na familia yake wanaishi ni kikubwa. Mbuga hiyo ya kitaifa imo kwenye ardhi ya upana wa nchi za Rwanda na Burundi ukizijumlisha pamoja- na kuna maji kidogo sana hasa wakati wa kiangazi. Wakazi waliruhusiwa kurejea kwenye ardhi yao lakini serikali haikuwaruhusu kuchimba visima. Wasan waliishtaki serikali tena – na mwaka 2011 wakashinda kesi hiyo pia. Serikali ilikubali uamuzi, lakini haikusaidia kuchimba visima vyovyote. Mashirika yasiyo ya Kiserekali pamoja na kampuni ya madini, Gem Diamonds ndio waliochimba visima. Visima hivyo vilichimbwa katika maeneo kadhaa, likiwemo eneo la Molapo.

Jumanda Gakelebone [*pron.* Ju-manda Ga-be-le-bo-ne] amekuwa kwa muda mrefu akishirikiana na Roy kupigania haki za raia wa San. Anaonyesha bomba lililo ardhini.

6. Clip Jumanda Gakelebone (English)

“Kisima hiki kilichimbwa mwaka uliopita na kampuni ya Gem Diamonds. Lakini hakikuwa na maji mazuri. Lau kisima hiki kingetoa maji, maisha ya watu yangebadilika. Watu walioondoka hapa mbugani wangerudi. Na matatizo ya nyakati za ukame yangekwisha.”

7. Narration

Visima vinne vilichimbwa katika mbuga, lakini ni eneo moja tu lililokuwa na maji yanayofaa binadamu. Na eneo hilo ni kilomita zaidi ya mia moja kutoka Molapo – mbali sana kwa watu wanaoishi katika makazi haya. Kwa hivyo, inawabidi wakinge maji ya kutosha wakati wa msimu wa mvua na watumie maji hayo mwaka mzima.

6. SFX: Field

Kommentar [s1]: Leider sehr leise!

8. Narration

Sithilo Thekiso [*pron.* Stilo Tekizo] ameketi chini akipumzika karibu na kisima katika Molapo. Anaendelea kujenga au kuzingira shamba ili azuie wanyama pori wasile mimea na mazao yao. Sawa na wakazi wengi wa Molapo, Sithilo amevaa fulana na suruali wala si mavazi ya asili. Sithilo alikuwa mwindaji, lakini serikali ilipiga marufuku uwindaji. Hata hivyo, alifanikiwa kurejea hapa hata baada ya kuhamishwa kwa nguvu.

9. Clip Sithilo Thekiso (San)

“Maisha yalikuwa magumu sana kwangu. Nikiwa hapa ninaweza kwenda nikajichimbia mizizi na pia ninaweza kupanda mimea ya mazao. Lakini katika eneo hilo jingine nisingeweza kufanya hivyo.”

10. Narration

Sithilo na mkewe, Mosalagadi Mowawaphuti [*pron.* Mota-hadi Mowa-puti] wanapenda maisha ya kienyeji, na wanaona kwamba Molapo ndipo mahali panapowafaa. Walifurahi si haba wakati mahakama ilipowaruhusu kurejea kwenye makazi yao. Hatimaye, anasema Mosalagadi, waliweza kuondoka eneo la New Xade [*tamka.* New Kadi], walimokuwa wamehamishiwa.

11. SFX: Women talking

Mama huyo aliye na watoto wanne anakaa chini mbele ya kijumba akiwa pamoja na wanawake wengine wa eneo hilo la makazi.

12. Clip Mosalagadi Mowawaphuti (San)

“Maisha ya New Xade yalikuwa tofauti na magumu kwangu. Ndiyo sababu nilirudi. Mtoto wangu mmoja ndiye aliyebaki huko. Namtamani sana binti yangu huyo, lakini sijui nitamfanya nini hata akubali kurudi hapa.”

13. Narration

Watu waliorejea kwenye mbuga hii hawafiki hata nusu ya idadi ya wale waliohamishwa kwa nguvu. Wengi waliorudi ni wazee na watoto. Binti ya Sithilo na Mosalagadi mwenye umri wa miaka 18 alibaki New Xade. Nilitaka kujua kisa na sababu iliyomfanya kubaki New Xade, ambayo ni moja miongoni mwa kambi tatu walikohamishiwa wakazi hao.

14. SFX: Car arrives

Kijiji hicho kiko mbali na mbuga ya wanyama na ni mwendo wa saa sita kwa gari. Katika kijiji hicho serikali imeweka muundo msingi wa kutegemewa: kuna hospitali, shule, na nyumba za wasimamizi. Watu wa jamii ya San waliohamishwa wanaishi katika vijumba vya kienyeji.

15. SFX: Women talking in New Xade

Hatimaye tunampata Bankganetse Sethilo [*pron.* Ban-ka-neti Stilo] katika kijumba kimoja cha kienyeji. Amekuwa akiishi hapa pamoja na bibi yake kwa muda wa mwaka mmoja. Hajakaa kama msichana wa kijijini; amevaa suruali ya kisasa ya kijeshi na fulana ya kisasa. Bankganetse anachanganyikiwa na anaona haya anaposema kwamba hataki kurudi kwao kijijni Molapo. Hataki kusema sana, lakini anasema kwamba marafiki zake wote wanaishi hapa New Xade.

Hiki kisa cha Bankganetse na jamaa zake kinabainisha mambo yanayoingilia maisha na utamaduni wa jamii ya leo ya Wasan. Ni vigumu sana kujumuisha maisha ya kienyeji ya uwindaji- uhamaji katika maisha ya kisasa. Katika makazi ya New Xade, wakazi Wasan kutoka Molapo walikumbana na maisha mapya. Walihudhuria shule, wakazoea maji ya bomba, na wakawa wakinunua mboga na vyakula kutoka dukani. Hata hivyo, mabadiliko hayo yaliwatatiza wengi. Mmoja wao ni Mabele Owa. Mzee huyo alilazimishwa kuhamia New Xade, lakini sasa hivi hataki kurudi kuishi katika mbuga ya wanyama.

16. Clip Mabele Owa (San)

“Nilikuwa mwindaji. Hapa sina lolote nifanyalo. Ninakaa na marafiki zangu na tunajiburudisha kwa kunywa kileo. Sina jambo niwezalo kufanya kusema kweli: haya ni kwa maisha yangu ya usoni, au ni kwa

maisha yangu, au wanangu. Nililazimishwa kuishi maisha haya, kwa hivyo nimekata tamaa.”

17. Narration

Jamaa zake wote wamerejea Molapo. Lakini Mabele ni mlevi. Huanza kunywa pombe yake haramu asubuhi – si yeye tu ambaye ni mlevi katika New Xade. Watu wengi hujaribu kujisahaulisha shida zao kwa kunywa pombe. Ni rahisi sana kuilaumu serikali kwa kila tatizo mtu alilo nalo. Nchi ya Botswana ina utajiri mwingi wa maliasili. Tofauti na nchi nyingine za Afrika, wenye uwezo ingawa wamejilimbikizia mali si haba, wamewekeza nchini mwao.

Lengu kuu la mpango huu wa kuwahamisha Wasan ni kuwapa elimu na pia huduma za afya. Bila shaka ni rahisi kutekeleza lengo hilo iwapo watakaa kwenye kambi za makazi kuliko kuzagaa kila mahali katika mbuga. Mwanaharaki wa Molapo, Roy Sesana, anafahamu lengo hilo. Lakini kwake yeye elimu na makazi ya asili ni mambo yaliyo na umuhimu sawa.

18. Clip Roy Sesana (San)

“Ningependa vitukuu vyangu viishi na kukamilishia maisha katika eneo hili. Kwa hivyo tunahitaji shule hapa, ambapo wanasomeshwa kwa lugha yao; ni lazima wafundishwe utamaduni wao. Na mwishoni mwa juma mama zao wanawafunza shughuli za kitamaduni, na baba zao wanawafunza jinsi ya kuwinda. Hatutaki kupoteza utamaduni; ni muhimu sana kwetu.”

19. Narration

Roy angependa wanawe wafahamu dunia zote mbili: hiyo ya huko mbugani, na pia maisha ya nje ya mbuga. Hapo basi watajiamulia wenyewe ni maisha gani bora kwao. Mwanaharakati huyu mwenye umri wa miaka 60 yuko tayari kupigania suala hilo- kama ambavyo amekuwa akifanya maishani mwake.

20. Clip Roy Sesana (San)

“Watu waliokandamizwa ni lazima wasimame kidete kutetea haki zao. Ardhi ni muhimu sana; ni sawa na baba na mama. Hapo ndipo ulipozaliwa, ndipo ulipokulia na ndio inayosababisha uwe jjiis ulivyo.”

Outro

Kauli hizo za mwanaharakati wa kutetea haki za Wasan, Roy Sesana, ndizo zinazotuhitimishia kisa cha leo cha **Noa Bongo Jenga Maisha**

Yako kutoka Botswana. Mwanahabari wetu alikuwa Adrian Kriesch.

Ukitaka kusikiliza taarifa nyingine za kipindi hiki kuhusu kuzingatiwa haki za jamii za walio wachache, tazama wavuti wetu dw.de/lbe. Usikose kututegea sikio katika kipindi kijacho. Kwaheri kwa sasa!